

Taarifa kuhusu rasilimali za kimatibabu na ushauri ndani ya bewa, na vile vile malazi yanayopatikana, zinaweza kupatikana kwenye: <https://www.tntech.edu/healthservices/>

Taarifa kuhusu mchakato wa kinidhamu wa wanafunzi zinaweza kupatikana kwenye: <https://www.tntech.edu/policies/>

Ndiyo. Taarifa kuhusu fafanuzi za jinai za jimbo lako za shamulizi la kimapenzi, dhuluma za kinyumbani, dhuluma za uchumba na ufuatiliaji mtu kwa njia isiyo ya kawaida zinaweza kupatikana katika Ripoti ya kimwaka ya Usalama: <https://www.tntech.edu/police/annual-security-report>

#### ***Visa ya U***

Kwa waathiriwa wa mashambulizi mabaya ya kimwili au kiakili kutokana na shughuli fulani ya kijinai, ikijumuisha shambulizi la kimapenzi, dhuluma za kinyumbani, kunajisiwa, mashambulizi, au matendo mengine husika ya jinai -Mwathiriwa/mtuma ombi ni lazima awe mwathiriwa wa shughuli ya kijinai inayohitimu na ana uwezekano wa kusaidia katika uchunguzi na/au kufungulia shughuli hiyo ya kijinai mashtaka  
-Kwa ujumla ni halali kwa miaka minne  
-Kwa taarifa zaidi, shauriana na mwanasheria wa uhamiaji, na utazame:

#### ***Visa ya T***

Kwa waathiriwa wa ulangazi wa binadamu -Ni lazima ukubali maombi kutoka kwa mamlaka za utekelezaji sheria ya ushirikiano katika uchunguzi au kufungulia mashtaka tendo/matendo ya ulangazi (isipokuwa uwe hauwezi kushirikiana kwa sababu ya kudhoofika

